**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**

**MTIHANI WA NUSU MUHULA WA KWANZAKIDATO CHA PILI**
**ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

1. Majibu ya swali la kuchagua

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | A | B | D | B | C | B | A | A | D |

2. Majibu ya swali la kuoanisha

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| G | B | A | E | C |

**SEHEMU B (Alama 70)**

3. Njia za kumtambua Allah (S.W)
   (i) Njia ya fitra
   (ii) Njia ya mazingira
   (iii) Vipawa alivyopewa mwanadamu
   (iv) Njia ya maumbile.

**[Hoja 4@ alama 2.5= 2.5x4 = Alama 10]**

4. Matapo ya fiqhi
   (i) Fiqhi Muamalat. Ni fiqhi inayojihusisha na mambo ya kijamii kama vile mirathi, mazishi, ndoa n.k
   (ii) Fiqhi Ibadati. Ni fiqhi inayojihusisha na mambo ya kiibada, kama vile swala, zakka, funga n.k.

**[Hoja 2@ alama 5= 2x5 = Alama 10]**

5. Sababu za Qur'an kuteremshwa kidogo kidogo
   (i) Kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na zilihitajia majibu ya kiwahyi.
   (ii) Ili kuwawezesha waumini wa mwanzo kuifahamu vizuri Qur'an na kuihifadhi vifuani kwa wepesi.

(iii) Ili Mtume (S.A.W) na Maswahaba waiingize Qur'an katika matendo kwa wepesi zaidi.
(iv) Iwe wepesi kwa Mtume Muhammad (S.A.W) kuufikisha ujumbe uliotangulian kwa ukamilifu kinadharia na kimatendo kabla ya ujumbe mwingine uliofuata.

**[Hoja 4@ alama 2.5= 2.5x4 = Alama 10]**

6. Mwenendo wa wenye kumfuata Mtume Muhammad (S.A.W) katika maisha ya kila siku.
   (i) Kumfanya Mtume (S.A.W) kiigizo katika maisha yao
   (ii) Kumtii Mtume (S.A.W) kwa kufuata yale aliyoagiza na kuacha yale yote aliyoyakataza
   (iii) Kumswalia Mtume (S.A.W) mara kwa mara na kila anapotajwa
   (iv) Kumsifu Mtume (S.A.W) kwa sifa zinazomstahiki.
   (v) Kumfanya Mtume (S.A.W) kuwa hakimu wa kutoa fat – wa juu ya maisha yao ya kila siku.

**[Hoja 4@ alama 2.5= 2.5x4 = Alama 10]**

7. Mambo anayofanyiwa mtu mara tu baada ya kufa
   (i) Kumfunga macho ikiwa alikufa macho yakiwa wazi
   (ii) Kumvua nguo zote
   (iii) Kumkogesha na kumpigisha mswaki
   (iv) Kulainisha viungo vyake ili visikakamae.

**[Hoja 4@ alama 2.5= 2.5x4 = Alama 10]**

8. Tofauti iliyopo kati ya swala ya maiti na swala ya kawaida.
   (i) Swala ya maiti haina rakaa lakini swala ya kawaida ina rakaa
   (ii) Swala ya maiti haina sijda wala rukuu lakini swala ya kawaida ina rukuu na sijda
   (iii) Swala ya maiti nni faradh kifaya lakini swala ya kawaida ni faradhi Ayn
   (iv) Swala ya maiti huswaliwa wakati wowote ambapo swala ya kawaida ina wakati maalumu.

**[Hoja 4@ alama 2.5= 2.5x4 = Alama 10]**

9. Kufafanua dhana za historia kwa mujibu wa Uislamu.

(i) Historian i kumbukumbu za matendo ya watu na matokeo ya matendo hayo katika maisha ya duniani na akhera.

(ii) Asili ya mwanadamu. Mwanadamu ameumbwa na Allah (S.W) kutokana na udongo na roho.

(iii) Lengo la kuumbwa mwanadamu ni kumuabudu Allah (S.W) katika maisha ya kila siku.

(iv) Lengo la kuumbwa ulimwengu na vyote vilivyomo ni kumtumikia mwanadamu.

(v) Hatma ya mwanadamu: Ni kufufuliwa baada ya kufa, na kulipwa kutokana na aliyoyatenda duniani.

**[Hoja 5@ alama 2= 2x5 = Alama 10]**

**SEHEMU C (Alama 15)**

10. Tofauti kati ya Zaka na Sadaka

(i) Zaka ni faradhi kwa mwenye uwezo wakati sadaka ni sunna.

(ii) Zaka ni hutolewa muda maalumu lakini sadaka hutolewa muda wowote

(iii) Zaka ni lazima ifikie nisab lakini sadaka hutolewa kiasichochote

(iv) Zaka hupewa watu maalumu lakini Sadaka hupewa mtu yeyote

**[Utangulizi alama 1.5, Hoja 4@ alama 3= 3x4 = alama12, Hitimisho alama 1.5, Jumla Alama 15]**